

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOA WA SIMIYU

Tel : 0282 981193

Fax : 0282 981194

Email : ded@busegadc.go.tz

Tovuti: www.busegadc.go.tz



Sanduku la Posta 157,
BUSEGA.

10 Disemba, 2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega kwa kushirikiana na AGPAHI anawatangazia nafasi za ajira kwa mkataba wa mwaka mmoja katika vituo vya kutolea huduma na tiba. Hivyo basi, Watanzania wote wenye Sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi zilizoainishwa hapo chini watume maombi.

1. MUUGUZI DARAJA LA II (Nafasi 1) - TGHS A

(a) Sifa za kuajiriwa

Kuajiriwa wenye cheti cha Uguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

(b) Kazi na Majukumu

- (i) Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.
- (ii) Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
- (iii) Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi
- (iv) Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani.
- (v) Kutoa ushauri nasaha
- (vi) Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
- (vii) Kutoa huduma za uzazi na afya ya mtoto
- (viii) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- (ix) Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
- (x) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

2. TABIBU MSAIDIZI (Nafasi 1) -TGHS A

(a) Sifa za kuingia moja kwa moja:

Kuajiriwa wenye Cheti cha Mtihani wa Taifa wa Kidato cha IV ambao wamehitimu Mafunzo ya Miaka Miwili ya Tabibu Wasaidizi (Clinical Assistants Certificate).

(b) Kazi na Majukumu:

- Kutoa huduma za Kinga na Tiba
- Kutambua na kutibu magonjwa
- Kutoa huduma ya Afya ya msingi (Primary Health Care)
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

3. DATA CLERK (Nafasi 1) - TGS D

(a) **Sifa za kuajiriwa**

Muombaji anapaswa kuwa na stahahada ya Juu au Shahada ya IT, twakwimu, au utunzaji wa kumbukumbu kwa njia ya ki elektroniki, awe na uzoefu wa takwimu za afya (Health, Data Experience), awe na uzoefu wa kutumia mfumo wa DHIS, EXCEL. MS ACCESS, PEI-INFO, SSP na uzoefu wa mifumo mingine itakuwa sifa ya ziada.

(b) **Kazi na Majukumu:**

- (i) utunzaji wa mfumo wa CTC, data base
- (ii) kuhuisha CTC data base
- (iii) kuingiza takwimu za wagonjwa kila siku na kutengeneza taarifa na kuwasilisha katika ngazi husika
- (iv) kurudisha faili za wagonjwa ambao hazijajazwa kwa mganga (clinical zirekebishwe)
- (v) kuhakikisha kila file la mgonjwa linakuwa na fomu ya kuchunguza ugonjwa wa kifua kikuu na magonjwa ya STI na kuhakikisha zinajazwa na mganga kila mgonjwa anapohidhuria kliniki
- (vi) kutengeneza mpango kazi wa kuboresha takwimu katika kituo husika katika mfumo wa CTC, data base na katika vyanzo vya Takwimu
- (vii) kuhakikisha matumizi sahihi ya mfumo unafanya kazi kila siku, kila waktati, kuhusisha nati virusi kila siku
- (viii) kuhakikisha unawasilisiliana na viongozi wako kwa wakati kwaajili ya kukarabati mfumo pindi tatizo linpotokea

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
2. Waombaji wote waambatishe nakala ya Cheti cha Kuzaliwa
3. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo binafsi (CV), nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
4. Picha moja Passport Size iandikwe jina kwa nyuma.
5. Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (**Statement of Results havitakubalika**)
6. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya kiingereza au Kiswahili na yatumwe kwa njia ya Posta kabla ya tarehe **19/12/2018** kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
S.L.P. 157
BUSEGA.



Eng. Mohamed S. Yamlinga
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Busega

MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
YAL MASHAURI YAWOJWA
BUSEGA